# IJUE THBUB: Kuanzishwa kwake, Muundo, Majukumu Mamlaka, Dira, Dhamira, Uwasilishaji Malalamiko

Talking notes for Radio programmes

Imeandaliwa na:

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere/Kilimani, S.L.P 1049,
DODOMA/Tanzania
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978
B/pepe: info@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz

**MADA 1**

# YALIYOMO


1.0 KUANZISHWA KWA TUME ........................................................1

2.0 MUUNDO WA TUME ...............................................................3

- 2.1 Uteuzi wa Makamishna ..........................................................3
  - 2.1.1 Sifa za uteuzi ..............................................................3
- 2.2 Uteuzi wa Katibu Mtendaji wa Tume ......................................5

3.0 MAJUKUMU YA TUME ...........................................................7

4.0 MAMLAKA NA MIPAKA YA UTENDAJI WA TUME .......................10

5.0 DIRA, DHAMIRA, TUNU NA MALENGO MKAKATI YA TUME .....11

- 5.1 Dira ya Tume .......................................................................11
- 5.2 Dhamira ya Tume .................................................................11
- 5.3 Tunu za Tume .......................................................................11
- 5.4 Malengo Mkakati ya Tume .....................................................12

6.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA MALALAMIKO TUME ...............12

- 6.1 Malalamiko Yanayofikishwa Tume ..........................................12
- 6.2 Njia za Kuwasilisha Malalamiko Tume ....................................13
  - 6.2.1 Kuandika barua .........................................................13
  - 6.2.2 Kufika kwenye ofisi za Tume .......................................15
  - 6.2.3 Kutuma ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani (SMS) ....16
- 6.3 Sababu za Lalamiko Kutoshughulikiwa na Tume ....................17
- 6.4 Malalamiko Ambayo Hayatachunguzwa na Tume ..................18
- 6.5 Hatua Zinazochukuliwa na Tume katika Uchunguzi wa Malalamiko ...........................................................................19

7.0 TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA MAHAKAMA ........................20

7.1 Mahakama ya Tanzania ........................................................ 20

7.1.1 Mfumo wa Mahakama Tanzania Bara ......................... 21

7.1.2 Mfumo wa Mahakama Zanzibar .................................. 22

7.1.3 Majukumu ya Mahakama ........................................... 23

7.2 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ........................ 25

7.2.1 Majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora .............................................................. 25

7.3 Uhusiano kati ya Mahakama na Tume ................................... 28

7.4 Tofauti zilizopo kati ya Mahakama na Tume katika utendaji kazi wa kila siku ..................................................................... 28

# 1.0 KUANZISHWA KWA TUME

THBUB ni taasisi inayosimama kama **chombo cha kitaifa cha haki za binadamu,** yaani 'National Human Rights Institution (NHRI)' na **chombo cha utetezi wa haki za jamii** (Ombudsman). Ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema, kutakuwa na Tume itakayoitwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. THBUB ni chombo huru cha Serikali kilichoanzishwa kwa lengo la kukuza, kulinda, kuhifadhi na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora hapa Tanzania.

Kuanzishwa kwa Tume hii kulitokana na mchakato wa mapendekezo ya Tume na Kamati mbalimbali, kama vile Tume ya Nyalali, Kamati ya Bomani, Kamati ya Kisanga na mapendekezo ya mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali.

Moja ya mapendekezo ya Kamati ya Nyalali ilikuwa kuanzishwa kwa chombo huru cha kusimamia haki za binadamu. Mapendekezo ya Kamati ya Bomani ya kurekebisha mfumo wa sheria (Legal Task Force) chini ya mpango wa kurekebisha mfumo wa kitaasisi na kisheria (FILMUP) kwenye ripoti ya mwaka 1996, moja ya mapendekezo yake ilikuwa ni kuanzishwa kwa Tume huru ya haki za binadamu na usimamizi wa utawala (Commission for Human Rights and Administrative Justice).

Kamati ya Kisanga ya kutafuta maoni ya wananchi kwa kutumia waraka wa Serikali Na. 1 wa mwaka 1998 (white paper No.1) kwa ajili ya kufanyia marekebisho Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya mwaka 1977, moja ya mapendekezo yake ilikuwa kuanzishwa kwa Tume huru ya kushughulikia haki za binadamu.

Hivyo, THBUB ilianzishwa kufuatia mabadiliko ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mabadiliko haya yalibadilisha Sura ya Sita (6) Sehemu ya Kwanza (1) ya Katiba iliyokuwa imeanzisha na kuelezea kazi za Tume ya Kudumu ya Uchunguzi iliyoanzishwa mwaka 1966 na kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo ilirithi pia majukumu na kazi za iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

Majukumu na kazi za Tume yamefafanuliwa zaidi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Sura ya Sita Sehemu ya Kwanza Ibara ya 130(1) na Kifungu Na. 6(1) cha Sheria ya Bunge ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura ya 391 ya Sheria za Tanzania.

THBUB kama Idara ya Serikali inayojitegemea, ni chombo cha Muungano kinachofanyakazi Tanzania Bara na Zanzibar. Ilianzishwa mnamo tarehe 01 Julai 2001 baada ya kupitishwa na kuanza kazi kwa Sheria ya THBUB Sura 391 ya Sheria za Tanzania na kutolewa kwa taarifa ya kawaida Na. 311 kwenye Gazeti la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 23 la tarehe 08 Juni 2001. Ilianza kazi rasmi Tanzania Bara tarehe 15 Machi, 2002 baada ya kuteuliwa na kuapishwa kwa Makamishna wake.

Aidha, THBUB ilianza kazi rasmi Zanzibar mwezi Aprili, 2007 baada ya Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuridhia na kupitisha Sheria ya THBUB na kuanza kufanya kazi kwa Sheria ya Nyongeza Na.12 ya 2003 (Extension Act No. 12 of 2003).

THBUB ilianza na watumishi wa Serikali 76 (63 Tanzania Bara, 13 Zanzibar) ambao walikuwa katika Tume ya Kudumu ya Uchunguzi, iliyofutwa kwa Sheria ya THBUB Sura 391 ya Sheria za Tanzania.

Tangu mwaka 2001/2002 Tume imekuwa ikiajiri watumishi wapya ili kukidhi mahitaji ya rasilimali watu. Hadi kufikia Desemba 31, 2019, Tume ilikuwa na jumla ya watumishi 154 katika nafasi mbalimbali, ikiwa ni pungufu ya watumishi 65 kufikia idadi ya watumishi 219 waliokuwa wanahitajika hadi kufikia mwaka wa fedha wa 2020/2021.

# 2.0 MUUNDO WA TUME

Ibara ya 129(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya THBUB Sura 391 ya Sheria za Tanzania vinafafanua kuwa Tume inaundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Makamishna watano na Makamishna Wasaidizi ambao ndiyo mamlaka ya usimamizi wa Tume.

## 2.1 Uteuzi wa Makamishna

### 2.1.1 Sifa za uteuzi

Ibara ya 129(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya THBUB Sura 391 ya

sheria za Tanzania vinafafanua sifa za mtu kuteuliwa kuwa Kamishna au Kamishna Msaidizi wa Tume.

Ibara ya 129(2) ya Katiba hiyo inasema, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itakuwa na Makamishna wafuatao:

- Mwenyekiti, ambaye atakuwa ni mtu mwenye sifa ya kuweza kuteuliwa kuwa Jaji;

- Makamu Mwenyekiti, ambaye atateuliwa kwa kuzingatia kanuni kwamba endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, yeye atakuwa ni mtu wa kutoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano;

- Makamishna wengine wasiozidi watano watakaoteuliwa kutoka miongoni mwa watu wenye ujuzi, uzoefu, na upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, sheria, utawala, siasa au mambo ya jamii;

- Makamishna Wasaidizi.

Aidha, Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya THBUB Sura 391 ya sheria za Tanzania kinasema, mtu mwenye sifa ya kuweza kuteuliwa kuwa Kamishna au Kamishna Msaidizi ni yule ambaye ana hadhi ya juu ya kuheshimika na anajulikana kuwa na kiwango cha juu kimaadili, uadilifu, kutenda haki (impartiality) na mwenye uwezo na uelewa mpana kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Ibara ya 129(3) ya Katiba hiyo na Kifungu cha 7(2) cha sheria hiyo vinafafanua kuwa, Makamishna na Makamishna Wasaidizi wote watateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi ambayo inapokea maoni kutoka kwa wananchi.

Ibara ya 129(5) ya Katiba hiyo na Kifungu cha 8(1) cha sheria hiyo vinafafanua kuwa, Makamishna wanafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu, na wanaweza kuteuliwa tena siyo zaidi ya kipindi cha pili kisichozidi miaka mitatu.

### 2.1.2 Kamati ya Uteuzi

Ibara ya 129(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema, kutakuwa na Kamati ya Uteuzi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

- Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani
- Spika wa Bunge
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi
- Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye atakuwa ndiye Katibu wa Kamati hii.

## 2.2 Uteuzi wa Katibu Mtendaji wa Tume

Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya THBUB Sura 391 kinasema, Tume itakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais baada ya mashauriano na Tume. Huyu ndiye msimamizi mkuu wa kazi za siku hadi siku kuhusu masuala ya kiutawala na utekelezaji wa maamuzi

ya kisera ya Tume.

Usimamizi wa kazi za siku hadi siku kuhusu masuala ya kiutawala na utekelezaji wa maamuzi ya kisera ya Tume umegawanywa katika Divisheni (Idara) na Vitengo. Kila Divisheni inaongozwa na Mkurugenzi, na kila Divisheni imegawanywa katika seksheni chini ya Wakurugenzi Wasaidizi. Divisheni hizo ni kama zifuatazo:

1. Divisheni ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu.
2. Divisheni ya Huduma za Kisheria
3. Divisheni ya Malalamiko na Uchunguzi
4. Divisheni ya Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka.

Aidha, kuna vitengo vifuatavyo katika Tume:

1. Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini
2. Kitengo cha Uhasibu na Fedha
3. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu
4. Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)
5. Kitengo cha Ununuzi na Ugavi.

Pia kwa ajili ya kurahisisha utendaji na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi Tume ina ofisi yenye hadhi ya kitaifa mjini Unguja – Zanzibar. Aidha, imefungua ofisi za matawi katika kanda nne (4) nchini. Ofisi hizo na maeneo zilipo ni kama ifuatavyo:

- **UNGUJA - ZANZÍBAR** (Ofisi yenye hadhi ya kitaifa), ipo katika jengo la Kamisheni la Wakfu na Mali za Amana, kitalu Na. 201, Mbweni.

- **DAR ES SALAAM** (Kanda ya Mashariki), ipo mtaa wa Luthuli, Kitalu Na. 8 katika jengo lijulikanalo kama "Haki House". Inapakana na iliyokuwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

- **MWANZA** (Kanda ya Ziwa), ipo mtaa wa Liberty, ndani ya jengo la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) Ghorofa ya tatu (3).

- **LINDI** (Kanda ya Kusini), ipo mtaa wa Wailesi, Barabara iendayo kwa Mkuu wa Mkoa, ndani ya jengo la zamani la TTCL.

- **WETE** (Kanda ya Pemba), mtaa wa Kitutia, mkabala na jengo la ofisi za posta Wete.

## 3.0 MAJUKUMU YA TUME

Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kifungu cha 6(1), vifungu vidogo (a) mpaka (o) vya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura ya 391 ya sheria za Tanzania vinafafanua majukumu ya Tume. Majukumu hayo ni:

a) Kukuza nchini kinga na hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;

b) Kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa ujumla;

c) Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

d) Kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

e) Inapobidi, kufungua mashauri mahakamani yanayolenga kukomesha ukiukwaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki zinapovunjwa au misingi ya utawala bora inapokiukwa;

f) Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote au taasisi yoyote ambayo vifungu vya sehemu hii vinahusiana navyo katika utaratibu wa kawaida wa kutekeleza kazi za ofisi yake au utendaji wa kazi unaokiuka mamlaka yake;

g) Kupeleleza au kuchunguza malalamiko yanayohusiana na utekelezaji au utendaji wa watu wanaoshikilia ofisi katika utumishi wa Serikali, mamlaka za umma au vyombo vya umma, ikijumuisha taasisi binafsi na watu binafsi ambapo malalamiko hayo yanadaiwa kuwa ni ya matumizi mabaya ya madaraka, huduma za upendeleo kwa mtu yeyote, ikiwa ni mlalamikaji au mtu mwingine, katika kutekeleza kazi zao za kiserikali au umma;

h) Kutembelea Magereza na mahala pengine wanamozuiliwa watu au sehemu zinazofanana kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanaozuiliwa sehemu hizo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hii;

i) Kuchukua hatua za kusaidia kusahihisha, kurekebisha, kuzuia au kukomesha vitendo vilivyotajwa katika vifungu (e), (f), (g) au (h) kutokana na njia za usawa, sahihi, na haki, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria;

j) Kutoa ushauri kwa Serikali na kwa vyombo vingine vya umma na taasisi za sekta binafsi juu ya mambo maalum yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora;

k) Kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwisha tungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakubaliana na haki za binadamu na za misingi ya utawala bora;

l) Kusaidia uridhiaji wa au utiaji saini mikataba au makubaliano yanayohusu haki za binadamu, kuzilinganisha sheria za nchi na kufuatilia na kutathmini utekelezaji ndani ya Jamhuri ya Muungano na Serikali na watu wengine, kwa viwango vya haki za binadamu vilivyoainishwa kwenye mikataba au makubaliano au chini ya sheria za kawaida za mahusiano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo;

m) Kwa kupitia Serikali, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika, Jumuiya ya Madola na taasisi nyingine zenye uhusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi za nje ambazo zina uzoefu katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu na utawala bora;

n) Kuchukua hatua zifaazo kwa ajili ya ukuzaji na uendelezaji wa upatanishi na usuluhishi miongoni mwa taasisi na watu mbalimbali ambao hufika au hufikishwa mbele ya Tume;

o) Kufanya kazi nyinginezo zozote kama zinavyoweza kuelezwa katika sheria nyingine.

## 4.0 MAMLAKA NA MIPAKA YA UTENDAJI WA TUME

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya THBUB Sura ya 391 ya sheria za Tanzania, vimetoa mamlaka na ukomo wa THBUB katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria hiyo kinafafanua kuwa THBUB itakuwa na mamlaka ya kufanya uchunguzi wa jambo lolote linalohusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Aidha, Ibara ya 131(2) ya Katiba hiyo na Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo vinafafanua kuwa THBUB haitachunguza mambo yafuatayo, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake, yaani:

- Jambo lolote ambalo liko mbele ya Mahakama au chombo kinginecho cha kimahakama;

- Jambo lolote linalohusu uhusiano au mashirikiano kati ya Serikali na Serikali ya nchi yoyote ya nje au Shirika la Kimataifa;

- Jambo linalohusu madaraka ya Rais kutoa msamaha;

- Jambo jingine lolote lililotajwa na sheria yoyote.

## 5.0 DIRA, DHAMIRA, TUNU NA MALENGO MKAKATI YA TUME

Mpango Mkakati wa THBUB wa miaka mitano (2018/2019 – 2022/2023) umeainisha dira, dhamira, tunu na malengo mkakati ya Taasisi kama ifuatavyo.

### 5.1 Dira ya Tume

Kuwa na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu, misingi ya utawala bora na utu wa mtu.

### 5.2 Dhamira ya Tume

Kuongoza ukuzaji, ulinzi na hifadhi ya haki za binadamu, misingi ya utawala bora na utu wa mtu kwa ushirikiano na wadau.

### 5.3 Tunu za Tume

- Kufanya maamuzi kwa uhuru
- Ushirikiano
- Uwazi
- Uadilifu
- Uwajibikaji
- Kuheshimu haki za binadamu
- Kutopendelea
- Usawa
- Mwelekeo wenye matokeo.

## 5.4 Malengo Mkakati ya Tume

Katika kipindi hiki cha miaka mitano (2018/19 hadi 2022/23) THBUB itatekeleza Malengo Mkakati yafuatayo:

- Kuboresha ulinzi wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

- Kuimarisha ukuzaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora na

- Kuboresha uwezo wa Tume katika utoaji huduma.

# 6.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA MALALAMIKO TUME

## 6.1 Malalamiko Yanayofikishwa Tume

Malalamiko yanayoweza kufikishwa Tume yanaweza kuwa katika maeneo yafuatayo:

- Uvunjwaji wa haki za binadamu;

- Ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

- Mwenendo wa mtu yeyote au taasisi yoyote katika kutekeleza madaraka au utekelezaji unaokiuka madaraka;

- Matumizi au matendo ya watu wenye madaraka katika utumishi wa Serikali kuu, Serikali za Mitaa (Vijiji/Kata/Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Majiji n.k), mashirika, makampuni ya umma,

vyombo binafsi na watu binafsi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, kutotenda haki au kuonea.

## 6.2 Njia za Kuwasilisha Malalamiko Tume

Kifungu cha 22(1 - 3) cha Sheria ya Tume Sura 391 ya Sheria za Tanzania kinaeleza utaratibu wa kuwasilisha malalamiko Tume. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa Tume na mtu mmoja, kikundi cha watu au taasisi. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo:

### 6.2.1 Kuandika barua

Mwandishi wa barua aandike jina kamili, anuani yake, namba ya simu, anuani ya baraua pepe (kama anavyo) na anuani ya mlalamikiwa ili Tume iweze kuendeleza mawasiliano na mlalamikaji/mlalamikiwa. Kwa kutegemeana na mahali alipo, mlalamikaji atatuma barua yake kwa kutumia mojawapo ya anuani zifuatazo:

**Mwenyekiti**
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P. 1049, DODOMA
Simu: 0734 047 775/ 0734 119 978
Barua  Pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

**Mwenyekiti**
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P. 285, ZANZIBAR
Simu: (024) 2230494/236124
Barua  Pepe: zanzibar@chragg.go.tz

**Mwenyekiti**
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P. 2643, DAR ES SALAAM
Simu: (022) 2135747/8
Barua  Pepe: dsm@chragg.go.tz

**Mwenyekiti**
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P. 10430, MWANZA
Simu: (028) 2541770; Fax (028) 2541770
Barua  Pepe: mwanza@chragg.go.tz

**Mwenyekiti**
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S.L.P. 1050, LINDI
Simu: (023) 2202734/2202744
Barua  Pepe: lindi@chragg.go.tz

**Mwenyekiti**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

S.L.P. 231, WETE - PEMBA

Simu: (024) 2454196

Barua Pepe: pemba@chragg.go.tz

### 6.2.2 Kufika kwenye ofisi za Tume

Mwenye malalamiko anaweza kufika katika mojawapo ya ofisi za Tume zifuatazo kuelezea malalamiko yake:

**DODOMA**

Mtaa wa Nyerere, Kitalu Na 339, Kilimani na UDOM, Kitivo cha Sayansi za Jamii na Biashara, zilipo Ofisi za Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria (Nyuma ya jengo zilipo Ofisi za Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ali maarufu "Utumishi."

**ZANZIBAR**

Jengo la Kamisheni la Wakfu na Mali za Amana, Kitalu Na. 201, Mbweni.

**DAR ES SALAAM** (Kanda ya Mashariki)

Jengo la Haki House – Mtaa wa Luthuli, inapakana na Jengo lililokuwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

**LINDI** (Kanda ya Kusini)

Mtaa wa Wailes, Jengo la zamani la TTCL, barabara ya kuelekea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

**MWANZA** (Kanda ya Ziwa)

Mtaa wa Liberty, Jengo la NBC, Ghorofa ya Tatu.

**WETE** (Kanda ya Pemba)

Mtaa wa Kitutia, Jengo linalopakana na Ofisi ya Posta, Wete.

### 6.2.3 Kutuma ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani (SMS)

Mwenye lalamiko au taarifa anaweza kutuma ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani kwenda **Na. 0737 446 787** kwa kufuata hatua zifuatazo:

**Jinsi ya kuwasilisha lalamiko…**

- Tuma lalamiko ukianzia na neno **'REPORT'** kwenda Na. **0737 446 787.Mfano:** *REPORT Shule ya Msingi Kinondoni DSM, tunachapwa viboko zaidi ya 10.*

- Utapokea ujumbe usemao lalamiko lako limepokelewa Tume, na utaelekezwa kama unayo maelezo zaidi yatume kupitia barua pepe: **info@chragg.go.tz** au piga simu Na.: **0734 047 775/ 0734 119 978.**

- Maafisa wa Tume wanaweza kukupigia simu ili kupata maelezo zaidi kabla ya kuanza kushughulikia lalamiko lako.

- Lalamiko lako litakapoanza kushughulikiwa, utapata ujumbe wa simu kukujulisha **Namba** ambayo utaitumia kufuatilia lalamiko lako. **Namba** hii itatumwa kwako kupitia namba ya simu uliyotumia kuwasilisha lalamiko lako.

- Utaweza kujua hatua ambayo maafisa wa Tume wamefikia kwa kutuma ujumbe wa simu pamoja na **Namba** ambayo utakuwa umepewa baada ya lalamiko lako kufunguliwa jalada.

**Jinsi ya kufuatilia lalamiko…**

Tuma ujumbe wako ukianza na neno **'STATUS'** kwenda Na. **0737 446 787**. **Mfano:** *STATUS 13024* (iwapo namba ya jalada lako utakayopewa ni 13024).

**Kumbuka:** Na. **0737 446 787** inapokea ujumbe tu, hivyo usipige simu kwenda namba hii, haitapokelewa.

## 6.3 Sababu za Lalamiko Kutoshughulikiwa na Tume

Kifungu cha 22(4) na (5) cha Sheria ya Tume Sura 391 kinasema, Tume itashughulikia kila lalamiko litakaloletwa kwake isipokuwa tu:

- Kama lalamiko limecheleweshwa kuletwa kwa kipindi kinachozidi miaka miwili tangu kuepo kwa lalamiko hilo. Hata hivyo Tume inaweza kuendelea kufuatilia au kuchunguza lalamiko hilo iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo;

- Kama mlalamikaji anayo nafasi ya kuelekeza lalamiko lake katika vyombo vingine vilivyopo na vyenye mamlaka kisheria;

- Lalamiko linatolewa kwa nia mbaya, bila ya sababu ya msingi au kwa nia ya kukomoa;

- Lalamiko liko nje ya mamlaka ya Tume;

- Kama lalamiko limetumwa kwa mamlaka nyingine na kunakiliwa Tume. Hata hivyo Tume inaweza kuendelea kufuatilia au kuchunguza lalamiko hilo iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

## 6.4 Malalamiko Ambayo Hayatachunguzwa na Tume

Kwa mujibu wa Ibara ya 131(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 16(2) cha Sheria ya Tume Sura 391 ya Sheria za Tanzania, THBUB haitachunguza malalamiko yafuatayo kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake:

- Lalamiko ambalo linashughulikiwa/ limeshughulikiwa na mahakama au chombo kingine chochote chenye asili ya kimahakama kama vile Baraza la Usuluhishi, Makazi n.k.;

- Lalamiko linalohusu mahusiano au mashirikiano kati ya Serikali na Serikali ya nchi yoyote ya nje au shirika la kimataifa;

- Lalamiko linalohusu madaraka ya Rais kutoa msamaha;

- Lalamiko ambalo Rais ameagiza vinginevyo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

- Malalamiko ya madai yatokanayo na mikataba binafsi, madai ya kawaida kwa mfano kuvunjika kwa ndoa, mirathi n.k.

## 6.5 Hatua Zinazochukuliwa na Tume katika Uchunguzi wa Malalamiko

Kifungu cha 19 – 27 cha Sheria ya THBUB Sura 391 ya sheria za Tanzania, vinaeleza utaratibu na hatua zinazochukuliwa na Tume katika uchunguzi wa malalamiko; baadhi ya hatua hizo ni pamoja na:

- Kuchukua hatua za kuhifadhi siri wakati wa uchunguzi wa malalamiko;

- Tume kukiri kupokelewa kwa malalamiko yaliyowasilishwa;

- Kuchambua malalamiko yaliyopokelewa kwa ajili ya kuyaainisha na sheria, kanuni, taratibu, mila, desturi, mazingira na wakati;

- Mlalamikaji au mlalamikiwa anaweza kuwakilishwa na wakili, mtu mwingine au ndugu katika kutoa maelezo, taarifa na nyaraka kama ushahidi kuhusu lalamiko linalochunguzwa;

- Tume inaweza kumtaka kwa maandishi mlalamikiwa kutoa taarifa, maelezo, nyaraka au vielelezo kuhusu malalamiko yanayochunguzwa. Vilevile kumtaka kwa maandishi mtu yeyote ambaye anafahamu juu ya malalamiko yanayochunguzwa kutoa taarifa, maelezo, vielelezo au nyaraka zitakazosaidia katika uchunguzi;

- Tume inaweza kutoa hati ya wito kwa mtu yeyote kufika Tume kwa ajili ya kutoa maelezo, taarifa, vielelezo, nyaraka na kuhojiwa kwa kiapo kwa ajili ya kusaidia katika uchunguzi wa malalamiko;

- Tume inaweza kutoa maelekezo kwa mtu yeyote kusitisha kwa muda matendo yanayoweza kuathiri uchunguzi wa malalamiko;

- Tume inaweza kuingia mahali popote kwa ajili ya kuchukua nyaraka, kumbukumbu na vielelezo ambavyo vitasaidia katika uchunguzi wa malalamiko;

- Baada ya uchunguzi Tume itamwarifu mlalamikaji juu ya ufumbuzi ambao umepatikana.

## 7.0 TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA MAHAKAMA

Mahakama na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni vyombo vilivyoundwa kwa mujibu wa Katiba na sheria ili viweze kufanya kazi ya kulinda, kusimamia na kutoa haki kwa wananchi pale zinapokiukwa.

### 7.1 Mahakama ya Tanzania

Mahakama ya nchi ni moja ya mihimili mitatu ya dola, Mahakama ina jukumu la kutoa haki kwa wananchi kwa kutoa maamuzi ya haki kwa mujibu wa sheria za nchi. Mihimili mingine ya dola ni Bunge na Serikali. Mahakama nchini Tanzania imegawanyika katika sehemu mbili. Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande mmoja (Tanzania Bara) na Mahakama ya Zanzíbar kwa upande wa

pili. Sababu ya kuwa na Mahakama pande zote mbili yaani, Mahakama ya Tanzania Bara na Mahakama ya Zanzíbar ni kuwa, suala la mahakama sio jambo la Muungano. Hivyo Zanzíbar ina mahakama yake na Tanzania Bara ina Mahakama yake, zote zina jukumu la kutafsiri sheria zinazotumika katika maeneo husika.

Hata hivyo, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ni jambo la Muungano. Mahakama hiyo ina uwezo wa kusikiliza rufaa kutoka pande zote za Muungano isipokuwa tu kwa yale mambo ambayo imenyimwa mamlaka ya kuyasikiliza kwa mujibu wa sheria.

### 7.1.1 Mfumo wa Mahakama Tanzania Bara

Mfumo wa Mahakama Tanzania Bara umeundwa na Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Majukumu ya Mahamaka hizo yameelezwa katika Katiba na sheria nyingine zilizotungwa na Bunge.

Mahakama Kuu ya Tanzania Bara ina vitengo vifuatavyo:


i) **Mahakama Kuu ya Kawaida** ambayo hupokea na kusikiliza kesi na rufaa yoyote isipokuwa kuhusu jambo ambalo kuna mahakama yake.

ii) **Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi** amabayo hupokea na kusikiliza kesi na rufaa zinazohusu ardhi tu kutoka Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

iii) **Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara** ambayo hupokea na kusikiliza kesi zinazohusu maswala ya biashara tu.

iv) **Mahakama Kuu Kitengo cha Ajira/Wafanyakazi** ambayo hupokea na kusikiliza kesi na rufaa zinazohusu maswala ya ajira tu kutoka Kamisheni ya Usuluhishi na Upatanishi.

#### 7.1.1.1 Muundo wa Mahakama ya Tanzania Bara





### 7.1.2 Mfumo wa Mahakama Zanzibar

Mfumo wa Mahakama Zanzibar umeundwa na Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu Zanzibar, Mahakama ya Mkoa, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Kadhi. Mahakama ya juu kwa upande wa Zanzibar ni Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mahakama ya Kadhi ina uwezo wa kusikiliza na kuamua mambo yote binafsi yanayohusu ndoa, mirathi, matunzo ya watoto, na zawadi kwa wanainchi wenye imani ya dini ya Kiislamu. Mashauri

yaliyoshughulikiwa na Mahakama ya Kadhi hayataweza kukatiwa rufaa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Mashauri mengine yote yaliyoamuliwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar yanaweza kukatiwa rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

#### 7.1.2.1 Muundo wa Mahakama ya Zanzibar




### 7.1.3 Majukumu ya Mahakama

- Mahakama ni chombo kilichopewa mamlaka ya kufanya maamuzi panapotokea migogoro baina ya pande mbili au zaidi kwa kubaini uvunjaji wa sheria uliojitokeza.

- Mahakama imepewa mamlaka na jukumu la kutafsiri sheria za nchi zilizowekwa.

- Mahakama ni chombo kinachopokea malalamiko, kuendesha kesi na kutoa hukumu. Mahakama hufanya jukumu hilo kwa:
  i) Kupokea malalamiko yanayohusu madai na jinai toka kwa mtu, taasisi yoyote au Serikali.

  ii) Kusikiliza malalamiko kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria.

  iii) Kutafsiri sheria zitakazotumika dhidi ya malalamiko.

  iv) Kutoa maamuzi juu ya malalamiko.

Mahakama haina wajibu wa kuwahamasisha walalamikaji kuwasilisha malalamiko kwake, bali husubiri mlalamikaji mwenyewe kuona umuhimu wa kudai haki yake mahakamani, aidha ni wajibu wa mlalamikaji kujua ni ngazi gani ya mahakama anapswa kuwasilisha lalamiko lake kulingana na asili ya lalamiko lake lilivyo. Asiporidhika na maamuzi yaliyotolewa anauhuru wa kukata rufaa kwenda Mahakama ya ngazi ya juu zaidi.

Uendeshaji wa kesi Mahakamani huambatana na gharama za uendeshaji kesi ambazo hupaswa kulipwa na mlalamikaji, ispokuwa tu kwa baadhi ya mashauri ya makosa maalum kesi zake hugharimiwa na serikali. Mfano kesi za mauaji.

## 7.2 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyofanyiwa marekebisho, na pia katika Sheria ya Tume Na. 7 ya 2001.

Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na katika kifungu cha 6(1) vifungu vidogo (a) mpaka (o) vya Sheria ya Tume. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

### 7.2.1 Majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

a) Kukuza nchini kinga na hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;

b) Kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa ujumla;

c) Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ;

d) Kufanya utafiti katika, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

e) Inapobidi, kufungua mashauri mahakamani yanayolenga kukomesha ukiukwaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki zinapovunjwa au misingi ya utawala bora inapokiukwa;

f) Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote au taasisi yoyote ambayo vifungu vya sehemu hii vinahusiana navyo katika utaratibu wa kawaida wa kutekeleza kazi za ofisi yake au utendaji wa kazi unaokiuka mamlaka yake;

g) Kupeleleza au kuchunguza malalamiko yanayohusiana na utekelezaji au utendaji wa watu wanaoshikilia ofisi katika utumishi wa Serikali, mamlaka za umma au vyombo vya umma, ikijumuisha taasisi binafsi na watu binafsi ambapo malalamiko hayo yanadaiwa kuwa ni ya matumizi mabaya ya madaraka, huduma za upendeleo kwa mtu yeyote, ikiwa ni mlalamikaji au mtu mwingine, katika kutekeleza kazi zao za kiserikali au umma;

h) Kutembelea Magereza na mahala pengine wanamozuiliwa watu au sehemu zinazofanana kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanaozuiliwa sehemu hizo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hii;

i) Kuchukua hatua za kusaidia kusahihisha, kurekebisha, kuzuia au kukomesha vitendo vilivyotajwa katika vifungu (e), (f), (g) au (h) kutokana na njia za usawa sahihi na haki, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria;

j) Kutoa ushauri kwa Serikali na kwa vyombo vingine vya umma na taasisi za sekta binafsi juu ya mambo maalum yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora;

k) Kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwishatungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakubaliana na haki za binadamu na za misingi ya utawala bora;

l) Kusaidia uridhiaji wa au utiaji saini mikataba au makubaliano yanayohusu haki za binadamu, kuzilinganisha sheria za nchi na kufuatilia na kutathmini utekelezaji ndani ya Jamhuri ya Muungano na Serikali na watu wengine, kwa viwango vya haki za binadamu vilivyoainishwa kwenye mikataba au makubaliano au chini ya sheria za kawaida za mahusiano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo

m) Kwa kupitia Serikali, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika, Jumuia ya Madola na taasisi nyingine zenye uhusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi za nje ambazo zina uzoefu katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu na utawala bora;

n) Kuchukua hatua zifaazo kwa ajili ya ukuzaji na uendelezaji wa upatanishi na usuluhishi miongoni mwa taasisi na watu mbalimbali ambao hufika au hufikishwa mbele ya Tume;

o) Kufanya kazi nyinginezo zozote kama zinavyoweza kuelezwa katika sheria nyingine.

## 7.3 Uhusiano kati ya Mahakama na Tume

Mahakama na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni vyombo ambavyo vinafanana sana katika utekelezaji wa majukumu yao katika jamii, kwakuwa:

i) Vyote ni vyombo vya kusimamia, kulinda, kuhifadhi na kutoa haki.

ii) Vyombo vyote vinahusika katika kutatua na kusuluhisha migogoro kati ya watu na mashirika, Serikali na kati ya mtu mmoja na mwingine.

iii) Vyote vinasimamia sheria.

iv) Vyote vina uwezo wa kuendesha kesi mbalimbali zinazohusiana na ukiukwaji wa haki.

## 7.4 Tofauti zilizopo kati ya Mahakama na Tume katika utendaji kazi wa kila siku

i) Mahakama ina jukumu la kutoa haki yoyote ile, iwe ya kisheria tu au haki ya binadamu kwa kufuata sheria za nchi. Mahakama ina uwezo wa kuamua kesi zote za madai na jinai bila ya kuingiliwa na chombo kingine chochote kile. Lakini, mamlaka ya Tume ni kuhusu mambo ya haki za binadamu na utawala bora tu.

ii) Mahakama huwa inatoa hukumu baada ya kusikiliza malalamiko yaliyowasilishwa mbele yake. Tume haina uwezo wa kutoa hukumu. Imepewa uwezo wa kutoa mapendekezo tu kwa Serikali au chombo kingine juu ya uvunjifu wa haki za binadamu na misingi

ya utawala bora. Na endapo mapendekezo yasipotekelezwa inaweza, ikiamua kufanya hivyo, kupeleka lalamiko mahakamani ili Mahakama iweze kusikiliza shauri hilo na kulitolea hukumu. (Tazama Sheria ya Tume Na. 7/2001, Kifungu cha 15(3)).

iii) Tume inafanya uchunguzi juu ya uvunjifu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora na kutoa mapendekezo. Mahakama haifanyi uchunguzi wa kesi, bali inasikiliza pande mbili zinazosigana kwa kupokea ushahidi toka pande hizo mbili na hatimaye kutoa hukumu kuwa ni upande upi umeshinda.

iv) Baada ya kufanya uchunguzi Tume haina uwezo wa kutoa adhabu kwa mkosaji, bali kutoa mapendekezo tu. Mahakama ina uwezo wa kutoa nafuu ya kisheria au adhabu kwa wakosaji baada ya kufikia maamuzi yake.

v) Katika Mahakama mlalamikaji anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya juu asiporidhika na hukumu ya Mahakama iliyo chini, lakini katika Tume hakuna muundo kama wa Mahakama.

vi) Tume inaweza ikaanzisha uchunguzi wake yenyewe bila ya kupata lalamiko toka kwa mtu yeyote (Tazama Sheria ya Tume Na. 7/2001, Kifungu cha 15(1)(a)). Mahakama haiwezi kushughulikia jambo lolote bila ya kuletwa mbele yake na mlalamikaji.

# # #